## .1.1 APPENDIX 4

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI-VETA

## CHUO CHA VETA SHINYANGA

S.L.P. 470 **SIMU**: 028-2763437. **FAX**: 028-2763200. **E- MAIL**: shinyangavtc@veta.go.tz.

### MAELEKEZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA CHUO CHA VETA SHINYANGA

1. **Unatakiwa kununua vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako ya chuoni**:
   i. Mashati mawili meupe (mikono mifupi)ya Tetron.
   ii. Suruali mbili za bluu ambazo utazikuta Chuoni kwa gharama ya **Tsh. 40,000/=** ambazo zitalipwa kwenye akaunti ya Chuo.
   **iii.** Ovaroli moja (bluu) kwa wanachuo wote isipokuwa kwa wanachuo wa fani za uhazili na Ushonaji utaikuta Chuoni kwa gharama ya **Tsh. 30,000/=.**
   iv. Ovacoati moja (nyeupe) kwa wanachuo wa fani za Uhazili, Ushonaji na Ung'arishaji vito **utaikuta Chuoni kwa gharama ya Tsh. 25,000/=.**
   v. Fulana ambayo utaikuta chuoni kwa gharama ya **Tsh.20,000/=.**
   vi. Sweta rangi ya bluu ambayo utaikuta Chuoni kwa gharama ya **Tsh. 15,000/=.**
   vii. Jozi moja ya **"safety boots"** (viatu vyeusi vyenye chuma mbele) pamoja na jozi moja ya viatu vya ngozi vyeusi vya kamba na visigino vifupi kwa wanafunzi wote isipokuwa kwa fani za ushonaji na Uhazili.
   viii. ***Kwa wanafunzi wa bweni wanatakiwa waje na mto, shuka,blanketi, chandarua, Godoro la size 2.5 x 6 kimo 4'' kwa wavulana na 3.5 x 6 kimo 4" kwa wasichana, bakuli, sahani, kikombe na kijiko, pamoja na ndoo au beseni la kuogea pamoja na vifaa vya usafi binafsi.***
   ix. *Vifaa vya hesabu (Mathematical set).*
   x. *Daftali 6 kubwa pamoja na vifaa vya uchoraji **(Technical Drawing)**.*
   xi. *Uje na nakala halisi ya vyeti.*

2. Unatakiwa kulipa kiasi cha fedha kama inavyoonyesha kwenye jedwali lifuatalo:-

***JEDWALI LINALOONYESHA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MBALI MBALI KWA MWAKA WA MASOMO WA 2023/24***

| S/N | MAELEZO | BWENI | | | KUTWA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | KWA MWAKA 1 | MHULA 1 | MHULA 2 | KWA MWAKA 1 | MHULA 1 | MHULA2 |
| 1 | SURUALI *2 | 40,000 | 40,000 | - | 40,000 | 40,000 | - |
| 2 | OVERALL/OVERCOAT | 30,000 | 30,000 | - | 30,000 | 30,000 | - |
| 3 | T - SHIRT* | 20,000 | 20,000 | - | 20,000 | 20,000 | - |
| 4 | SWETA* | 15,000 | 15,000 | - | 15,000 | 15,000 | - |
| 5 | NEMBO YA VETA*2 | 5,000 | 5,000 | - | 5,000 | 5,000 | - |
| 6 | MAHAFALI | 40,000 | 40,000 | - | 40,000 | 40,000 | |
| 7 | BIMA YA AFYA | 50,400 | 50,400 | - | 50,400 | 50,400 | - |
| 8 | PESA YA TAHADHALI | 10,000 | 10,000 | - | 10,000 | 10,000 | - |
| 9 | KITAMBULISHO | 5,000 | 5,000 | - | 5,000 | 5,000 | - |
| 10 | MICHEZO* | 10,000 | 10,000 | - | 10,000 | 10,000 | - |
| 11 | ADA YA MAFUNZO* | 60,000 | 60,000 | - | 60,000 | 60,000 | - |
| 12 | ADA YA MTIHANI* | 25,000 | - | 25,000 | 25,000 | | 25,000 |
| 13 | ADA YA BWENI* | 60,000 | 60,000 | - | - | - | |
| | JUMLA | **370,400** | **345,400** | **25,000** | **310,400** | **285,400** | **25,000** |

***NB:-***

- ✓ ***Malipo yote yatalipwa kupitia Mfumo wa GEPG.Hivyo Control namba yako inapatikana ufikapo Chuoni.***
- ✓ ***Fedha ikishalipwa hairudishwi, isipokuwa fedha za tahadhari (caution money).***

***Viambatanisho:-***

1. *Sheria za Chuo.*
2. *Medical Examination form (**Vipimo vifanyike katika Kituo cha afya au Hospitali za serikali tu)***
3. *Fomu ya kuthibitisha kujiunga na chuo (**ijazwe na kurudishwa Chuoni kabla ya tarehe ya kufungua)***

*SHERIA ZA CHUO*

***Ili kufanikisha mafunzo ya awali ya ufundi kila mwanafunzi anatakiwa kufuata sheria zifuatazo:-***

1. ***MAHUDHURIO***
    a) *Kila mwanafunzi anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1.15 asubuhi.Hii ina maana saa 1.15 wanafunzi wote wawe chuoni.**Adhabu kali itatolewa kwa wachelewaji**.*
    b) *Mwanafunzi hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani,Hospitali au sehemu nyingine yoyote ile bila ya kibali cha Mkuu wa Chuo.*
    c) *Mwanafunzi apatapo matatizo ya msiba,kuuguliwa au kuugua mwenyewe ni lazima habari/taarifa zifike chuoni, bila ya kufanya hivyo ni kosa.*
    d) *Mahudhurio chini ya 85% mwanafunzi hataruhusiwa kufanya mtihani wa kuhitimu mafunzo.*
    e) *Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake. Hairuhusiwi kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.*

2. ***MAVAZI***
    a) *Sare ya chuo ni suruali ya Bluu na shati jeupe mikono mifupi.Sare hiyo ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo chuoni na wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani isipokuwa siku za Jumatano na Ijumaa mwanachuo ataruhusiwa kuvaa Fulana (t-shirt). Wakati wote shati liwe limechomekewa.*
    b) *Ovaroli au Overcoat zivaliwe wakati wa vipindi vya kazi za mikono tu.*
    c) Viatu vyenye visigino virefu na kandambili au viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni.

3. **USAFI WA MWILI**
    a) Hairuhusiwi kuvaa hereni,Pete,bangili, mkufu na mapambo ya aina yoyote ile kwa kipindi chote cha mafunzo.Hairuhusiwi kutumia vipodozi au manukato yanayotoa harufu kali.

    b) **Nywele kwa wavulana**
        (i) Zikatwe ziwe fupi na isiwe KIPARA.
        (ii) kufuga ndevu hairuhusiwi kabisa.

**c) Nywele kwa wasichana**

(i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni).

**d) Kucha ndefu haziruhusiwi kabisa wala kupakwa rangi.**

4. **WIZI WA MALI ZA CHUO AU MALI YA MTU YEYOTE YULE:**
   a) Vitendo vyovyote vya wizi haviruhusiwi. Pindi ikibainika mwanafunzi ameiba mali ya chuo au ya mwanafunzi mwenzake, hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.
   b) Ukipoteza kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe.
   c) Hairuhusiwi mwanafunzi kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo.
   d) Mwanafunzi atapekuliwa wakati wa kutoka karakana na getini.

5. **UGOMVI:**

   Ugomvi, kupigana na kushambuliana ni makosa ya jinai.Atakayepatikana akijihusisha na matendo ya namna hiyo hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja.

6. **ULEVI**

   Iwapo itabainika mwanafunzi amelewa au kuonekana katika sehemu za kileo,
   anavuta bangi au madawa ya kulevya hatua za kisheria zitachukuliwa mara moja juu yake.

7. **MAPENZI**
   a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya mwanafunzi na mwafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanafunzi hauruhusiwi kabisa.
   b) Mwanafunzi wa kiume au wa kike haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.
8. **MIGOMO:**

   Migomo ni mafuruku, na kuchochea migomo ni kosa lisilostahimilika.
   Atakayeshawishi au kusababisha migomo hatua za kisheria zitachukuliwa
   mara moja.

9. **LUGHA**:

   Lugha inayotumika kuendeshea masomo ni kiingereza hivyo ni wajibu wa kila mwanafunzi kujifunza kiingereza.
10. Hairuhusiwi kubadilisha jina la mwanafunzi mpaka ziwepo sababu na hati maalum kwa uthibitisho na kibali cha Mkuu wa Chuo.
11. Ni Marufuku kwa mwanachuo kuja na simu ya mkononi chuoni.

## ONGEZEKO LA SHERIA KWA MWANACHUO WA BWENI

12. Mwanachuo ataruhusiwa kutoka nje ya chuo siku zifuatazo tu:
    i) Jumamosi tangu saa 7.30 mchana hadi saa 12.00 jioni.
    ii) Jumapili na siku za sikukuu tangu saa 12.00 asubuhi hadi 12.00 jioni.
    iii) Hairuhusiwi kutoka nje ya chuo wakati wowote bila kibali maalumu.
13. Mwanachuo yeyote anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la Chuo anapaswa kuwa na sare ya chuo, kitambulisho cha Chuo na atajiandikisha lango kuu.Mwanafunzi atakayekiuka masharti tajwahapo juu, atachukuliwa hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa nafasi ya bwenini au kufukuzwa Chuoni.
14. Mwanafunzi atakayepatikana na kosa la kulala au kuwa nje ya chuo bila kibali atasimamishwa masomo na kupoteza sifa ya kuishi bweni.
15. Hairuhusiwi kupika chakula bwenini au eneo la Chuo atayekiuka sheria hii atachukuliwa hatua kali.
16. Ni marufuku wanachuo wa kiume na wakike kutembeleana mabwenini.
17. Hairuhusiwi kupeleka chakula Bwenini.Endapo kuna mgonjwa,ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu itatolewa.
18. Hairuhusiwi kupokea au kuingiza chakula chochote ndani ya Chuo kutoka nje ya chuo isipokuwa kwa kibali maalumu.
19. Taa za madarasani na mabweni zizimwe saa 4:00 za Usiku.
20. Hairuhusiwi kumkaribisha au kumlaza mgeni bwenini, ikiwa mwanachuo atatembelewa na mgeni siku ya masomo ni lazima kumjulisha mwalimu wa zamu kabla ya kumkaribisha katika sehemu ya mazungumzo.
    - Wageni wanaruhusiwa kuwatembelea ndugu zao kila Jumamosi kuanza saa 7:00 mchana hadi saa 12:00 jioni.
    - Kila Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka 12:00 jioni.
21. Hairuhusiwi kulala nje ya Chuo.Iwapo ikitokea ruhusa itatolewa na ofisi ya Mkuu wa Chuo.

**APPENDIX 5**

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi………………………………………………….ninakubali nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa pamoja na kuzingatia sheria na kanuni za chuo ambazo nimezisoma na kuzielewa vizuri.

Saini:……………………………………..……… Tarehe:……………………………………..

**b) MDHAMINI**

Mimi………………………………………….. ambaye……………………………………………wa mtajwa hapo juu nathibitisha kuwa nitamdhamini na nitamlipia gharama zote za mafunzo ikiwa ni ada na michango mingine kama ilivyoelezwa katika maelezo ya kujiunga na chuo wakati wote wa mafunzo.

Saini:……………………………………..……… Tarehe:……………………………………..

*Mawasiliano yote ya kiofisi yatumwe kwa Mkuu wa Chuo*

**APPENDIX 6**

# VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY

## MEDICAL EXAMINATION FORM

**Date:…………………………………….**

The Medical Officer

……………………………………………

……………………………………………

……………………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of trainee:……………………………………………..

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training subsequently work as a/an…………………………………………………

i. Hearing…………………………………………………...
ii. Eyesight…………………………………………………
iii. Asthma……………………………………………………..
iv. Other serious disease……………………………...

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit for training as above.

Date:…………………………………...      Designation:……………………………………..……………..

Signature & Official Stamp………………………………………………

**……………………………………………………………………………………………………………………………………………….**